BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

<u>BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI</u>

<u>MKUTANO WA KUMI NA MBILI</u>

<u>Kikao cha Nane – Tarehe 22 Septemba, 2023</u>

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. <u>HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:</u>

**<u>Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:</u>**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2022/2023.

**<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:</u>**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto juu ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

18. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Pamoja na juhudi za Halmashauri na Mabaraza ya Miji za kusafisha miji na vijiji vyetu ili nchi yetu ilete haiba nzuri, bado tuna tatizo kubwa la uhaba wa magari ya kuchukulia majitaka. Kwa mfano Pemba nzima ina gari moja tu ambayo inahudumia Mikoa yote miwili. Hali kama hii ya uhaba huo pia inapatikana katika Halmashauri na Mabaraza ya Wilaya za shamba.

    Je, Wizara ina mpango gani wa kuzipatia magari ya maji taka Halmashauri na Mabaraza yetu ya Miji, ili kuondokana na athari za uchafu wa maji taka mijini na vijijini mwetu.

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

61. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    (a) Ingawa Sheria inatambua uwepo wa wafanyakazi majumbani lakini ni lini Wizara itawajengea wafanyakazi hawa utaratibu wa kuwarasimisha ili iwe ni sehemu ya ajira na mikataba yao kutambulika kihalali.

    (b) Ni kwa namna gani Wizara yako inasimamia haki za wafanyakazi wa majumbani na inatumia utaratibu upi wa kuthibitisha kuwa hawakoseshwi stahiki zao.

    (c) Je, Wizara yako inawasimamia vipi wafanyakazi hao ili na wao wawajibike ipasavyo kwa waajiri wao.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

7. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

   Hivi sasa kuna changamoto kubwa ya vitendo vya ushoga na ndoa za jinsia moja ambavyo vimekithiri duniani na kuenea katika nchi zetu za kiafrika ikiwemo Tanzania.

   Je, Serikali ina mikakati gani katika kupambana na vitendo hivyo vya ushoga na ndoa za jinsia moja, vitendo ambavyo ni kinyume na mila na desturi zetu za kizanzibari na kitanzania kwa ujumla.

52. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

   (a) Je, tunakitumia vipi Kiswahili katika kukuza diplomasia ya nchi yetu kikanda na kimataifa

   (b) Je, ni upi mchango wa vyombo vya habari katika kukikuza na kukieneza Kiswahili Sanifu (Kiunguja Mjini).

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

5. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

   Viongozi wa ulinzi na usalama pamoja na walimu hupangiwa kusimamia uendeshaji wa mitihani ya Taifa maskulini katika Mikoa yote ya Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2022 viongozi hao waliwajibika ipasavyo katika kuimarisha ulinzi na usalama ili kuhakikisha malengo ya Serikali ya mitihani hiyo kumalizika kwa salama hasa Wilaya ya Kaskazini “A”.

   (a) Je, kuna utaratibu gani wa kuwapatia malipo viongozi hawa kwa utendaji wao wa kazi.

   (b) Je, kwa kiasi gani Wizara yako inafahamu kuwa malipo yanayosemwa kuwa yameshalipwa, hadi hii leo bado hayajawafikia viongozi na walimu wa Mkoa wa Kaskazini “A” Unguja.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

34. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Maonesho ya kilimo ya Nane Nane yamekuwa yakiwavutia na kuwapa hamasa wananchi wengi kujiingiza katika uzalishaji wa mazao ya kilimo badala ya kutosha tu kuwa watizamaji.

    Je, Wizara ina tathmini yoyote juu ya mafanikio ya wananchi kushajiika kuekeza kwenye kilimo baada ya kufika na kujionea wenyewe maonesho hayo.

93. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Kilimo cha mpunga ni kilimo ambacho wananchi wetu wa Zanzibar wanakitumia ili kujikwamua na changamoto ya chakula. Pamoja na juhudi hizo, wananchi wetu hushindwa kufikia malengo kutokana na kutonyesha mvua pamoja na mabonde yenyewe kuchoka.

    (a) Je, Serikali ina mpango gani wa nchi mzima wa kuwasaidia wakulima kwa kuyaingiza mabonde yao kwenye mfumo wa umwagiliaji.

    (b) Kwa kuwa miongoni mwa mashamba ambayo yanastahiki kutupiwa macho ni pamoja na mashamba yaliyomo ndani ya jimbo la Wingwi. Je, Mhe Waziri unawaambia nini wananchi wa Wingwi juu ya kuyaboresha mashamba yao na kuwa ya mfumo wa umwagiliaji.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

45. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

    Je, ni lini Wizara itawatumia wabunifu waliopo Zanzibar, wenye uwezo wa kutengeneza umeme wa gesi kwa kutumia maganda ya mazao mbali mbali, ili kupunguza gharama za gesi ya kawaida.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Ripoti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2022/2023.

**Zanzibar,**
**22 Septemba, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**